# Falsafa ya Maisha katika Ushairi wa Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert

*Angelus Mnenuka*

*Ikisiri*

Kutofautiana kimawazo ni miongoni mwa sifa muhimu sana za binadamu. Sifa hii inasahauliwa na watu wengi kiasi cha kuwafanya washangae inapotokea watu wakiwa na mawazo yanayotofautiana. Binadamu ana akili inayoweza kubuni vitu mbalimbali vinavyokubalika na wengi au vinavyokubalika na baadhi tu ya watu. Tofauti za binadamu hujitokeza katika maeneo mbalimbali mojawapo ni katika kazi za kubuni ambapo mtunzi wa kazi anaweza kueleza hisia na mawazo yake au kuwakilisha mawazo ya watu wengine kulingana na matakwa yake. Makala haya yanachunguza mitazamo kuhusu dhana ya maisha na mustakabali wake kama inavyoelezwa na Shaaban Robert na Mugyabuso Mulokozi. Tutachunguza ili kubaini kufanana na kutofautiana kwa mitazamo yao. Aidha, makala yataeleza chanzo na misingi ya tofauti hizo, pamoja na kufanana kwao.

## 1.0 Utangulizi

Miongoni mwa sanaa pekee ambayo msanii na mwandishi wa fasihi huelezea hisia zake za ndani zisizoweza kuelezeka katika lugha ya kawaida ni ushairi (Beaty na wenzie, 2002). Kwa kawaida hisia hizo huathiriwa kwa kiasi kikubwa na mazingira anamoishi msanii kwa sababu akili na uzoefu wa mwandishi vinachongwa na kuathiriwa na mazingira yanayomzunguka kama nadharia ya Umarx inavyodai (Barry, 2002). Vilevile, msanii huathiriwa na huiathiri jamii kwa namna mbalimbali (Vázquez, 1973). Hata hivyo, mazingira na makuzi havimzuii msanii kutunga au kuandika mawazo mapya kabisa ambayo hayapo katika jamii inayomzunguka kwa sababu msanii ana hisia na akili yenye uwezo wa kuibua mawazo mapya yaliyo nje ya mazingira yanayomzunguka (Finnegan, 1977 na Okpewho, 1992).

Makala haya yanachunguza mawazo ya malenga wawili wa Kiswahili ambao ni Shaaban Robert na Mugyabuso Mulokozi, kuhusu namna wanavyoyatazama maisha. Tumeamua kuwalinganisha malenga hawa kwa sababu kubwa mbili. Mosi, ni wasanii wanaoandika ushairi uliotofautiana kifani. Hii ina maana kwamba wakati Shaaban Robert ameandika mashairi mengi kwa kufuata urari wa vina na mizani, Mugyabuso Mulokozi ameandika mashairi mengi ya kisasa ambayo hayafungwi na urari wa vina na mizani.[1] Pili, Shaaban Robert ni

[1] Ingawa Mulokozi na Kahigi (1979) wanadai kuwa hata Shaaban Robert alitunga ushairi usiozingatia urari wa vina na mizani, basi tunaamini kuwa Shaaban Robert aliegemea zaidi katika urari wa vina na mizani kuliko ushairi huru.

mwenyeji wa maeneo ya Mashariki mwa Tanzania na ameishi miaka ambayo nchi ilikuwa ikitawaliwa na wakoloni wa Kijerumani na wa Kiingereza. Shaaban Robert ameutumia muda mrefu wa maisha yake katika kutumikia serikali ya kikoloni; Mugyabuso Mulokozi ni mwenyeji wa kanda ya ziwa na ameishi katika kipindi ambacho nchi ya Tanzania imepitia hatua kubwa na muhimu ambazo zimeacha athari kadha wa kadha katika sanaa mbalimbali. Baadhi ya vipindi hivyo ni kipindi kilichotawaliwa na sera ya Ujamaa (1967 – 2000) na baadaye sera ya soko huria (2000). Kutokana na tofauti hizo kubwa, tutaangalia mitazamo yao kuhusu maisha na mustakabali wake.

Shaaban Robert[2] ni mtunzi maarufu wa kazi za fasihi ya Kiswahili. Shaaban Robert, anaweza kuitwa Shakespeare katika fasihi ya Kiswahili japokuwa hakufanikiwa kuandika tamthiliya. Mugyabuso Mulokozi[3] kwa upande wake ni mwanazuoni na mtafiti wa utamaduni na fasihi ya Kiswahili, na Kiafrika kwa ujumla.

## 2.0 Dhana ya Maisha kwa Ujumla

Maana na dhana ya maisha na mustakabali wake ni miongoni mwa masuala yaliyowasumbua na yanaendelea kuwasumbua wanafalsafa na wataalamu mbalimbali kwa sababu ya kutokukubaliana. Hii inadhihirisha kuwa mawazo yanayotolewa bado hayawaridhishi wataalamu hao na umma wote kwa ujumla. Baadhi ya watu mashuhuri duniani ambao wameathiri mitazamo mikubwa kuhusu maisha na mustakabali wake ni pamoja na Gautama Siddhartha

[2] Historia fupi ya maisha ya Shaaban Robert imeandikwa na Yusuf Ulenge na John W.T. Allen katika kurasa za mwanzo za baadhi ya vitabu vya Shaaban Robert. Baadhi ya vitabu hivyo ni *Almasi za Afrika* (1972), *Mapenzi Bora* (1969), *Mashairi ya Shaaban Robert* (1968), na *Mwafrika Aimba* (1969). Aidha, ufupisho wa sifa nyingi zaidi zimefafanuliwa vizuri na Aaron L. Rosenberg katika makala yake ya *Making the Case for Popular Songs in East Africa: Samba Mapangala and Shaaban Robert.* Hata hivyo, taarifa za Rosenberg (2008) zinatofautiana na zile zilizotolewa na Yusuf Ulenge pamoja na Abdulrahim Hussein Taib katika makala yake ya *Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi* iliyochapishwa katika jarida la Mulika Na. 28 (2009). Wakati Roserberg akidai kuwa Shaaban Robert alitokea katika Ukristo, Yusuf Ulenge na Taib (2009) wanadai kuwa alitokea katika Uislamu kama Taibu (2009:131) anaposisitiza, "Juu ya yote hayo, Shaaban bin Robert alikuwa ni Muislamu bin Muislamu bin Muislamu. Hakupatikana katika ukoo wake ama kuumeni, ama wa kukeni kwake asiyekuwa Muislamu." Baadhi ya vitabu vilivyoandikwa na Shaaban Robert ni *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini, Kusadikika, Wasifu wa Siti Binti Saad, Masomo yenye Adili, Insha na Mashairi, Kielezo cha Fasili, Sanaa ya Ushairi, Utubora Mkulima, Siku ya Watenzi Wote, Mashairi ya Shaaban Robert, Mwafrika Aimba, Almasi ya Afrika, Adili na Nduguze*, na *Ashiki Kitabu hiki.*

[3] Amefanya tafiti mbalimbali na kuzichapisha katika muundo wa vitabu na makala ambazo ni hazina kubwa kwa wanafunzi wa sekondari, vyuo na vyuo vikuu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilimpa uprofesa wa fasihi kutokana na kazi yake kubwa katika utafiti wa fasihi nchini Tanzania na ukanda wa Afrika Mashariki kwa ujumla. Maeneo ambayo amebobea ni ushairi, riwaya na tamthiliya. Aidha, Profesa Mulokozi anafuatilia kwa makini ujitokezaji wa fasihi simulizi za jadi katika fasihi pendwa ya Kiswahili. Licha ya kufanya tafiti, Mugyabuso Mulokozi ameandika kazi kadhaa za ubunifu ambazo, tukiachilia mbali mashairi, ameandika riwaya za *Moto wa Mianzi, Ngome ya Mianzi,* na *Ngoma ya Mianzi.*

anayefahamika kama Buddha (?563-?483 KK), Confucius (551-479 KK) kwa upande wa Mashariki ya mbali; Yesu (?0-?33 KK) na Muhammad au Mohammed (?570-632 BK) kwa upande wa Mashariki ya Kati, Democritus (460-? KK), Plato (?427-347 KK), Socrates (?470-399 KK) na Aristotle (384-322 KK), John Locke (1632–1704 BK), Georg Wilhelm Friedrich Hegel (1770-1831 BK), Karl Marx (1818-83 BK) Søren Aabye Kierkegaard (1813-55 BK) kwa upande wa nchi za Magharibi. Sheria, mitazamo na maisha ya watu wa Ulaya na Marekani vimeathiriwa na mawazo ya wanafalsafa hao waliotajwa hapo juu, kama ilivyo kwa mifumo ya maisha ya watu wa Mashariki ilivyoathiriwa na falsafa za baadhi ya wataalamu tuliowataja hapo juu, na hata Mashariki ya Kati. Afrika, kwa upande wake, imeathiriwa kwa kiasi kikubwa na ontolojia za jamii zao pamoja na wanafalsafa walioathiri Ulaya na Marekani pamoja na Mashariki ya Kati kupitia ukoloni wa (Kiarabu na Kizungu kwa viwango tofauti. Kwa hiyo, barani Afrika kuna watu walioathiriwa na ontolojia za jamii zao, wanafalsafa wa Mashariki ya Kati kama vile Yesu na Muhammad na wapo wale walioathiriwa na wanafalsafa wa Mashariki ya mbali na Ulaya na Marekani, na wapo wale walioathiriwa na mchanganyiko wa falsafa hizo kwa kujua au kutokujua. Athari hizi zinajitokeza pia katika kazi za sanaa, hususan fasihi. Ili kuufanya mjadala wetu uwe rahisi, hatuna budi kuchambua kipengele kimojakimoja. Kwa hiyo, mjadala wetu utagawanyika katika vipengele kadhaa kama inavyofafanuliwa hapo chini.

## 2.1 Maisha ni nini?

Kama ilivyodokezwa hapo awali, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojadiliwa na wanafalsafa wengi bila kupata mwafaka. Swali hili linajadiliwa pia na wanafasihi wa Kiswahili, wakiwemo Shaaban Robert na Mugyabuso Mulokozi.

Kwa mujibu wa Mulokozi, maisha ya binadamu huanza pale anapozaliwa na huishia pale anapofariki dunia. Lakini kujibana katika sentensi hiyo ni kutoa maana finyu ya maisha na kutomtendea haki msanii huyu. Mugyabuso Mulokozi anafasilije maisha kwa upana wake? Mulokozi anaamini kuwa dunia imekaliwa na watu wenye hulka mbalimbali. Wapo wale wapenda haki, usawa na udugu; vilevile wapo wale wenye hulka ya ugandamizaji, uonevu, unyonyaji, na unyanyasaji dhidi ya wengine. Kwa hiyo, maisha ni mapambano baina ya wanyonge, watu wanaopigania haki na usawa dhidi ya wagandamizaji, wanyonyaji na wanyanyasaji.

Kwa kuwa maisha ya binadamu huanza na huishia hapahapa duniani, maisha ni mapambano ya wanyonge kujitetea wenyewe kwa upande mmoja, na wagandamizaji kuimarisha tabaka lao ili waendelee kunufaika na vitendo vyao

vya unyonyaji. Kwa hiyo, wanyonge wanapaswa kujipigania kwa sababu hakuna nguvu nyingine wala msaada kutoka nje ya dunia na upeo wa mwanadamu unaoweza kuwasaidia kuondoka katika tabaka hilo. Hata hivyo, anasisitiza kuwa hatua ya kupambana haitokei kirahisi, suala muhimu kuliko yote kabla ya mapambano ni urazini kama anavyoeleza katika shairi lake la *Mkulima*:

*Na mimi hubaki nikijiuliza*
*Kuna siri gani inamliwaza?*
*Au kujua au kutojua?*
*Furaha ya mtu ni furaha gani*
*Katika dunia inayomhini?*
*Ukali wa jua wamnyima zao* (*Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, uk. 67)

Ubeti huu unaonesha wasiwasi wa mwandishi kuhusu urazini wa mkulima kama kweli anabaini kuwa ananyonywa na anajua kuwa uwezo wa kubadili hali hii umo ndani yake mwenyewe.

Tatizo la kutotambua nguvu waliyonayo watu wa tabaka linalogandamizwa na kunyanyaswa ndio hasa mkingo wanaotumia wanyonyaji, ikiwa ni pamoja na wale wenye madaraka, kumgandamiza mkulima watakavyo. Ikiwa wanyonywaji watatambua nguvu walizonazo basi wataanzisha mapambano dhidi ya wanyonyaji popote walipo, kama ni dola basi dola hiyo itapinduliwa ili kuondoa unyonyaji. Mawazo haya yanapatikana katika shairi la *Siku Yetu* anapoonesha kuwa pindi watu wanaonyonywa wakitambua kuwa wana uwezo wa kupambana na wanyonyaji wao watafanikiwa anaposema:

*Siku hiyo ikifika mwenzetu,*
*Utatambuwa kuwa twaweza kitu,*
*Ukisulubiwa na kula mtutu,*
*Wala usififuke siku ya tatu!* (*Malenga wa Bara*, uk. 80).

Kwa hiyo, maisha ni zaidi ya kuzaliwa, kuishi na kufa. Ni lazima binadamu anayeishi apiganie haki na stahili yake kwa sababu havipatikani bure tu. Kwa ujumla, Mugyabuso Mulokozi amejionesha bayana kuwa si mtu anayeamini kuwa haki na stahili ya mtu, au mafanikio ya mnyonge yanaweza kupatikana kirahisirahisi tu bila nguvu, au siku moja wanyonyaji kuamua kuacha unyonyaji na kuanza kutoa haki. Wakati Mugyabuso Mulokozi akiamini hivyo, Shaaban Robert anaamini kuwa haki ni suala jema na anadai kuwa pakiwepo haki basi dunia itakuwa sehemu nzuri ya kuishi kama wazo hilo linavyojitokeza katika shairi lake la *Haki*.

*HAKI ni jambo aula, walimwengu kutumia,*
*Haki dawa ya madhila, nuru katika dunia,*
*Na pindi ikitawala, udhalimu hukimbia* (*Mashairi ya Shaaban Robert*, uk.1).

Pamoja na kutambua umuhimu wa haki, msanii huyu hadokezi njia za kuipata haki hiyo kana kwamba mtu anaweza kupewa haki bila kuidai. Badala yake, katika shairi lake la *Mbegu za Mungu* anadai kuwa anayetenda haki anampendeza Mungu, na anayefanya vitendo vya dhuluma anajiharibia mbingu kama ubeti huu katika shairi la *Mbegu za Mungu* unavyosema:

*Dhuluma mbaya, haina [M]zungu,*
*Wa kufikia mbele ya Mungu,*
*Haitafaa katika mbingu* (*Mashairi ya Shaaban Robert*, uk. 19).

Kwa hiyo, Shaaban Robert anashindwa kudokeza suluhisho la kudai haki kwa nguvu kama Mugyabuso Mulokozi kwa sababu anaamini kuwa kuna nguvu nyingine ya kimetafizikia inayoweza kudhibiti vitendo hivyo kwa kutoa thawabu na adhabu kwa wale watendao haki na wasiotenda haki katika maisha hapa duniani. Pamoja na kutambua kuwepo unyonyaji katika dunia, Mugyabuso Mulokozi anaamini kuwa mifumo yote ya kinyonyaji siku moja itasambaratika na wanyonywaji watashika hatamu kama inavyojitokeza katika mashairi ya *Maombolezo ya Mtu Maskini* (MB), *Siku Itafika* (MB), *Kauli ya Madhulumu* (MB), na *Enzi za Mapambano* (KUD). Kwa mfano, katika shairi la *Siku Itafika* mshairi anasema:

*Siku hiyo itafika, itafika, itafika,*
*Siku yao watu fyeka, kuinuka, kuinuka*
*Wale wanaomenyeka, kuanza kupumzika,*
*Siku hiyo itafika, itafika, itafika* (*Malenga wa Bara*, uk. 24)

Kwa kifupi, Mulokozi anaamini kuwa uovu upo lakini kamwe hauwezi kuushinda usawa na haki. Matendo yote ya unyanyasaji na ugandamizaji yana mwisho, haviwezi kudumu milele. Kama haviishi leo basi wale watakaofuata wataishi katika dunia yenye usawa na haki. Wazo hilo pia linapatikana katika shairi la *Japo Vingi vina Mwisho* kama ifuatavyo:

*Japo haya hutokea ulimwenguni tulimo,*
*Mimi bado nafikiri Muda hanao uwezo*
*Kufunika jamalayo itoweke kimokimo:*
*Moyo wa upendo wenye uthabiti*
*Utulivu wako wenye tahadhari*
*Hamasa ya kazi makini ya dhati*
*Kiburi cha haki penye ujeuri*
*Muhanga kwa wana kwa mume na nti*
*Ukuu wa roho, nia na nadhari* (*Kunga ya Ushairi na Diwani Yetu*, uk. 82)

Wazo hili linafanana na mawazo yaliyofafanuliwa na mwanafalsafa wa Afrika ya Kaskazini wa zama za kati Mt. Augustino (354-430) anayedai kuwa uovu ni

matokeo ya wema kupotea, yaani, kilichokuwepo kwa asili ni wema, lakini uovu hutokea pale tu wema unapotoweka (Calder, 2007). Kwa hiyo, kwa kuwa wema, haki na usawa vipo na unyanyasaji, dhuluma, na ugandamizaji vimejitokeza baadaye, basi kuna uwezekano mkubwa wa uovu kupotea kuliko wema kutokomea kabisa. Tunaweza kusema kuwa mawazo hayo ni sehemu ya mtazamo wa maisha kwa mujibu wa Mulokozi.

Mtazamo wa maisha wa Shaaban Robert hautofautiani sana na ule wa Mulokozi wa kuyatazama maisha kama sehemu inayokaliwa na watu wenye tabia mbalimbali mbaya na nzuri. Kuna mashairi mengi yanayodokeza wazo hilo, kama vile *Kitandawili cha Dunia, Tumeharibika, Ulimwengu* na *Dunia*. Kutoka katika vitabu vya *Insha na Mashairi* na *Almasi za Afrika*. Tuangalie mfano kutoka katika ubeti wa pili wa shairi lake la *Ila* kama ifuatavyo:

*Huimba Mwezi na Jua,*
*Umasikini na Mali,*
*Au Bahari na Hewa;*
*Hari na Baridi kali,*
*Na Fahari na Ukiwa,*
*Na Haramu na Halali;*
*Na Milima ya kukwea,*
*Na Mito na Majabali* (*Insha na Mashairi*, uk. 45)

Katika shairi hilo na mengine yaliyotajwa hapo juu, Shaaban Robert anadokeza kwa ufupi pande mbili zinazosigana katika maisha hapa duniani. Kuna maskini lakini pia kuna wenye mali, kuna haramu lakini pia kuna halali. Ameeleza baadhi ya tofauti za msingi za maisha ya watu hapa duniani kuwa, binadamu wametofautiana katika maisha. Kwa hiyo, kuhusiana na tofauti za watu hapa duniani malenga wote wanafanana. Hata hivyo, tofauti kubwa inayojitokeza baina ya Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert ni namna ya kuzisawazisha tofauti hizo. Wakati Mugyabuso Mulokozi anapendekeza mapambano dhidi ya wanyonyaji, wanaoishi maisha ya kifahari kwa kuwanyonya wengine; Shaaban Robert anaonekana kuathiriwa sana na imani ya kidini kiasi cha kujikuta akiangukia katika mkondo unaoamini kuwa kila kitu duniani hutokea kwa sababu kimepangwa na Mungu, ambapo binadamu hana uwezo wa kubadilisha mipango hiyo. Kwa hiyo, tajiri alifanywa hivyo na Mungu hali kadhalika maskini, kama Mungu hakupanga jambo fulani litokee, basi hakuna uwezekano wa jambo hilo kutokea. Wazo hili linapatikana katika shairi lake la *Pato* kama anavyosema:

*Kikubwa au kidogo mgawaji wetu ni Mungu,*
*Naye hatwishi mizigo mizito mizito wala michungu,*
*Juu yao walimwengu begani yenye msago* (*Mwafrika Aimba*, uk. 12).

Ubeti huu wa shairi unasisitiza mipango ya Mungu na unaondoa uwezekano wa mtu kutoa lawama au visingizio kwa Mungu kuwa ana matatizo makubwa kwa sababu, Shaaban Robert anasema kuwa, Mungu hamtwishi mtu mzigo mzito. Ni mtazamo usio na kanuni za kisayansi na hivyo ni vigumu kuuthibitisha kwa njia za kawaida za kibinadamu. Wazo hilo linajitokeza pia katika shairi lake la *Tulivyo* kama linavyosomeka hapo chini:

*Haji duniani mtu apendavyo,*
*Wala haondoki kama atakavyo,*
*Hanayo hiari ya kufanya hivyo,*
*Hawezi kusema kuwa hivi sivyo,*
*Lakini Mwenyezi ni aamruvyo* (*Mwafrika Aimba*, uk. 35).

Kwa ujumla, mawazo ya mkondo huu anaotumia Shaaban Robert unaondoa kabisa hamasa za watu kuleta mapinduzi wakiamini kuwa wamekuwa hivyo kwa sababu Mungu ameamua wawe hivyo. Hata hivyo, katika baadhi ya mashairi, Shaaban Robert anasisitiza jitihada za mtu mmojammoja katika kupambana na umaskini ili kila mtu aishi maisha bora. Kwa mfano, katika shairi la *Kazi*, Shaaban Robert anasema:

*MTU asiyejituma, mwenyewe na kwa ujira,*
*Hapati zawadi njema, mjinga hana busara[,]*
*[Siku zote] huwa nyuma, na wenziwe humbera,*
*Milele hana tijara mlegevu wa huduma* (*Mashairi ya Shaaban Robert*, uk.1).

Pamoja na kufanana katika kutambua matatizo hapa duniani, na utatuzi wake kwa kufanya kazi na matendo mema, Mugyabuso Mulokozi anaenda mbali zaidi na kudai kuwa ili kuondoa hali hii, yanahitajika mapinduzi. Mapinduzi ya wale wanaonyonywa kuondoa mfumo wa unyonyaji, ilhali, Shaaban Robert hagusii wazo la kufanya mapinduzi akiamini kuwa mwenye mali anaweza kushuka chini siku moja na maskini anaweza kupata mali siku moja kadiri ya mapenzi ya Mungu. Wakati Mugyabuso Mulokozi akitazama mapinduzi dhidi ya wanyonyaji ndio njia pakee ya kuondoa unyanyasaji na dhuluma katika jamii, Shaaban Robert anaona njia muhimu ya kuleta amani na afueni ya kimaisha hapa duniani ni kumwomba Mungu. Wazo hili linajitokeza katika mashairi yake kadhaa kama vile shairi la *Okoa Wanadamu* kama ubeti huu unavyodhihirisha wazo hilo:

*Mungu mtenda mambo,*
*Okoa wanadamu,*
*Maisha yao tambo,*
*Na daima magumu* (*Mashairi ya Shaaban Robert*, uk. 20).

Wakati Mugyabuso Mulokozi akiamini kuwa siku ya wanyonyaji kuondolewa mifumo ya kinyonyaji itakufa kama tulivyoona katika mashairi yake ya *Siku Yetu Kauli ya Madhulumu, Siku Itafika,* na *Enzi za Mapambano;* Shaaban Robert haoni uwezekano huo kama tulivyosema na kama anavyosisitiza katika shairi la *Mnyonge* hapa chini:

*Usemavyo sisadiki,*
*Naona ni neno geni,*
*Mnyonge kupata haki,*
*Wanifanyia utani.*
*Mnyonge hana rafiki,*
*Jamaa wala jirani.*
*Mkiwa mwenzie dhiki,*
*Siku zote duniani* (*Mwafrika Aimba,* uk. 9).

Kipande cha mwisho cha mstari wa shairi hili kinaonyesha namna gani Shaaban Robert alivyozama katika mkondo unaoamini kuwa duniani kuna mfumo uliowekwa ambao binadamu hana nafasi yoyote ile ya kuubadilisha. Kwa kifupi kabisa, tofauti kubwa baina ya Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert kuhusu maana ya maisha inajitokeza katika kutazama upeo na uwezo wa mwanadamu katika kubadilisha maisha yake mwenyewe, mifumo aliyoikuta au inayomzunguka na kubadilisha sheria za kimaumbile za dunia.

Hata hivyo, malenga hawa wanafanana katika kuona umuhimu wa mashujaa. Wote wawili wanatoa sifa kwa mashujaa na wote wawili wameandika mashairi yanayomhusu Mtwa Mkwawa wa Uhehe. Kwa upande wa Shaaban Robert, mawazo hayo yanajitokeza katika mashairi ya *Kufua Moyo*, shairi linaloelezea umuhimu wa ujasiri na ushujaa, na shairi la *Mkwawa* linaloelezea ushujaa wa Mkwawa na kutokana na ushujaa wake bado anaendelea kukumbukwa hadi hivi leo. Kwa upande wake Mulokozi anawasifu mashujaa mbalimbali katika shairi lake la *Kwa Mutwa Mukwava na Mashujaa Wengine* ambapo anamtazama Mkwawa kama ishara ya ufunguo wa ukombozi wa Mwafrika kupinga ukoloni.

## 2.2 Chanzo cha Maisha ni nini?

Kwa mujibu wa Mugyabuso Mulokozi maisha ya binadamu huanza duniani na huishia duniani, yaani huanza pale uhai unapoanza na huisha pale binadamu anapofariki dunia. Jambo hili limefafanuliwa katika shairi lake la *Mimi ni Nani* kama ifuatavyo:

*Mimi ni nani?*
*Niko wapi?*
*Nimetoka wapi?*
*Ninakwenda wapi?*
*Wengi watajibu:*

*Mimi ni mtu,*
*Niko duniani*
*Nimetoka ardhini*
*Ninakwenda mbinguni;*
*Bali mimi nasema;*
*Mimi ni kitu*
*Niko ardhini*
*Nitarudi ardhini* (*Kunga ya Ushairi na Diwani Yetu* na *Mashairi ya Kisasa* kur. 76 & 31)

Kama ubeti huu unavyoeleza, chanzo cha maisha kwa mujibu wa Mugyabuso Mulokozi ni ardhi, yaani hapahapa duniani. Tunadhani neno "ardhi" limefumbata dhana nyingine nyingi ambazo hazijafafanuliwa na mshairi. Tukumbuke kuwa watu hawaokotwi ardhini wala hawapatikani chini ya ardhi. Kwa hiyo dhana ya ardhi katika ubeti huu wa shairi imebeba wazo kubwa zaidi. Ikumbukwe kuwa zaidi ya jua, ardhi ni kitu muhimu kinachomuwezesha binadamu kuishi. Kutokana na ardhi binadamu anakunywa maji, anakula mazao na matunda mbalimbali, na anapata madini mbalimbali yanayomsaidia kiafya na kiuchumi. Yote haya ni mazao ya ardhi. Wanyama wanaotegemewa kwa chakula, shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, hutegemea ardhi yenye rutuba inayostawisha majani na mimea ambayo ni chakula cha wanyama. Kutokana na maelezo haya binadamu anaishi kutokana na ardhi na anaendelea kupata uzao kutokana na ardhi; hivyo binadamu anatokana na ardhi kwa sababu bila ardhi hakuna binadamu. Kwa kifupi tunaweza kusema kuwa kwa mujibu wa Mulokozi, maisha huanza pale uhai unapotungwa kwa wazazi ambao uhai wao hutegemea ardhi. Kwa mantiki hiyo, mtu yeyote anayeharibu ardhi, kwa mujibu wa Mulokozi, anatishia uhai wa binadamu na viumbe wengine wote.

Aidha, dai kuwa ardhi ni chanzo cha uhai wa binadamu linaenda sambamba na wazo linalodokezwa katika shairi hilohilo ambapo msanii huyu amepinga uwepo wa Mungu na dhana zinazoandamana nazo. Kupinga uwepo wa dhana ya Mungu na dhana zinazoandamana nazo kama vile shetani, malaika, mbingu na jehanamu, dhana zinazoaminiwa na wengi kuhusishwa na uhai wa binadamu, kunatoa nafasi ya kutafuta mwelekeo mwingine unaofafanua chanzo cha maisha ya binadamu. Kwa kifupi, Mugyabuso Mulokozi anamtazama binadamu kama kiumbe mwenye welewa mkubwa wa kubuni mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubuni uwepo wa Mungu, malaika, shetani, mbingu na jehannamu. Kwa mujibu wa Mulokozi, binadamu hana tofauti na wanyama wengine, na hivyo, muda mfupi baada ya kufa anaanza kuoza na kuwa sehemu ya udongo.

Shaaban Robert kwa upande wake, anaamini kuwa binadamu anazaliwa kama baadhi ya wanyama wengine lakini mipango hiyo ya kuzaliwa inapangwa na

Mungu. Hii inatokana na hoja zinazojengwa na mkondo anaoutumia ambao ndio hasa unafafanua kila kitu, yaani kuamini kuwa binadamu hana uwezo wa kufanya kitu kwa uhuru wake kwa sababu kila kinachotokea kinapangwa na Mungu[4]. Hatutaki kurudia ufafanuzi uliotolewa hapo juu, bali tunataka kuonesha kuwa Shaaban Robert anaamini kuwa kabla na baada ya kuzaliwa uhai wa mtu hauko mikononi mwa binadamu, bali kuna uwepo mkubwa zaidi unaoweza kuamua kuwepo au kutokuwepo kwa binadamu, yaani kama ni mtoto, azaliwe au asizaliwe, aishi au afe, kama ataishi aishi kwa muda gani na afanye nini akiwa hapa duniani, wazo hili linapatikana katika shairi lake la *Tulivyo* kama tulivyokwishakuona hapo juu. Wazo hili linajitokeza pia katika shairi lake la *Mwanzo na Aheri* anapotoa wazo la jumla kuhusu ualfa na uomega wa Mungu kwa kila kitu duniani kama shairi linavyosema:

*BARA na bahari vilivyomo vyote,*
*Mwenyewe Kahari ulimwengu wote,*
*Hanayo chanjari pahali popote,*
*Wa kwenda urari wakati wowote (Insha na Mashairi,* uk. *27).*

Mshairi huyu anatuambia kuwa Mungu ndiye mwanzo wa kila kitu, ikiwa ni pamoja na binadamu, yaani kutungwa mimba, kuzaliwa, kuishi na hatimaye kufa. Mawazo hayo tunayaona pia katika shairi lake la *Jalala* ambapo anaelezea ukuu wa Mungu katika kutoa uhai au kuuondoa kama anavyosema:

*MWANA sijampa jina, amefariki ghafla,*
*ni kaziye Maulana, sina werevu na hila,*
*nakuomba Mungu Bwana, ipe pazuri mahala,*
*Rohoyo huyu kijana, samehe dhana na ila (Almasi za Afrika,* uk. *52).*

Kama tulivyodokeza hapo awali, mkondo wa falsafa ambao ameegemea ni ule unaoamini kuwa binadamu hana nafasi ya kuathiri chochote duniani bila idhini au nguvu kutoka kwa Mungu, anaamini kuwa kifo cha mtoto ambaye hakubahatika hata kupata jina ni mapenzi ya Mungu. Kwa hiyo, binadamu anaishi na kuongozwa na uwepo ambao unamzidi nguvu kwa kila kitu. Uwezo huo unaitwa Mungu.

Tofauti na Mugyabuso Mulokozi anayedai, kama tulivyoona hapo juu, kuwa binadamu anazaliwa na kuishi kwa kutegemea matunda ya ardhi. Baada ya kuzaliwa binadamu huishi kulingana na mazingira yanayomzunguka mpaka atakapopata uwezo wa kujitegemea. Kufanikiwa kwa binadamu kunatokana na

---

[4] Mtazamo huu umejadiliwa na wataalamu mbalimbali ndani na nje ya dini ya Kiislamu kama anavyofafanua Patton (1900).

yeye mwenyewe, watu wengine, au vyote kwa pamoja; halikadhalika kuanguka kwake. Hakuna nguvu nyingine nje ya binadamu inayoweza kuathiri maisha yake kwa namna yoyote ile, si shetani, si malaika wala si Mungu. Kwa hiyo, tofauti iliyopo ni kwamba Shaaban Robert anaamini kuwa uhai wa binadamu kwa ujumla wake, kabla na hata baada ya kuzaliwa huongozwa na Mungu. Mugyabuso Mulokozi anaamini kuwa mifumo yote ya uzazi na makuzi haihusiani hata kidogo na Mungu, yote yapo chini ya uwezo wa binadamu.

### 2.3 Baada ya Kufa nini Kinatokea?

Kutokana na tofauti kadhaa zilizojitokeza hapo juu, tumeona vyema kuchunguza pia mitazamo ya wasanii hawa kuhusu hali inayotokea baada ya kifo. Kutokana na vidokezi vichache ambavyo tumeviona hapo juu tuna hakika kuwa wasanii hawa watakuwa na mawazo tofauti kuhusu dhana ya kifo na hasa hali inayomtokea binadamu baada ya kufa.

Mugyabuso Mulokozi, na kama ilivyojitokeza katika baadhi ya mashairi yake yaliyodondolewa hapo juu, anaamini kuwa maisha ya binadamu yanaanza na yanaishia hapahapa duniani. Kwa hiyo, kama ilivyo kwa viumbe hai wengine, baada ya kufa binadamu huoza na kuwa udongo. Ndio ukomo wa maisha ya binadamu. Mawazo haya yanajitokeza katika mashairi yake ya *Mimi ni Nani, Kalale Mwenyewe* na *Nikifa*. Kama tulivyokwishakudokeza hapo awali kuwa, katika mashairi ya Mugyabuso Mulokozi, dhana ya Mungu haipo, na kwa hakika anapinga kuwa hakuna nguvu inayomwongoza binadamu nje ya binadamu mwenyewe. Mfano mzuri ni shairi lake la *Mimi ni Nani*? Anaeleza bayana kuwa hakuna Mungu, hakuna malaika wala shetani, na kwamba baada ya kufa binadamu wote huoza na kuwa udongo, wakati huohuo akitoa wazo mbadala wa dhana hizo zinazotajwa kama shairi linavyoeleza:

*Bali mimi nasema:*
*Mimi ni kitu*
*Niko ardhini*
*Nimetoka ardhini*
*Nitarudi ardhini*
*Hakuna Mungu*
*Hakuna mbingu*
*Hakuna shetani*
*Hakuna malaika* (*Kunga ya Ushairi na Diwani Yetu* na *Mashairi ya Kisasa* kur. 76 & 31)

Mugyabuso Mulokozi anaamini kuwa maisha ya binadamu yanaanza na yanaishia hapahapa duniani hakuna sehemu wala hali nyingine aipatayo binadamu baada ya kufariki dunia. Kwa kifupi, baada ya kufa binadamu huoza, na huo ndio mwisho wa historia ya binadamu. Kama alidhulumiwa na

kunyanyaswa akiamini kuwa angepata maisha mazuri baada ya kifo, basi amedanganyika. Vilevile, kama amefanya matendo kadha wa kadha akiamini kuwa angepata faida katika ulimwengu mpya baada ya kifo, hatapata, angalau atakuwa amewasaidia baadhi ya watu kwa matendo mema aliyotenda, suala ambalo ni zuri.

Msimamo huo wa kutokuwa na maisha baada ya kifo bila shaka ndio unaomfanya Mugyabuso Mulokozi kupinga kwa dhati mifumo yoyote inayoonyesha dalili za unyonyaji baina ya watu katika maisha. Anayedhulumiwa na kunyonywa duniani, maana yake yupo *jehanamu* maisha yake yote, kwa kuwa hana nafasi nyingine ya kuishi. Tunaweza kusema kuwa falsafa ya mwanzo na mwisho wa maisha ya Mugyabuso Mulokozi ndiyo inayotumika kufasili maisha na namna ya kuishi duniani.

Wakati Mugyabuso Mulokozi akisema hayo, Shaaban Robert anadai kuwa kuna nguvu inayomwongoza binadamu na kwamba binadamu hana uwezo wa kufanya chochote bila nguvu hiyo, ambayo inaitwa Mungu na dhana zinazohusiana naye. Kwa mfano, katika shairi lake la *Dua Langu na Letu* anataja baadhi ya sifa za Mungu kama ifuatavyo:

*Mungu hushindwi na neno,*
*wala kwa kuniokoa,*
*hushindwi na magombano,*
......................................
*Na milele Mwabudiwa,*
......................................
*Tuongeze na juhudi,*
*uvivu usituvize.*
*Mbele yako tusujudi,*
*Shetani asiziweze,*
*Roho zetu kufisidi, ....*(*Almasi za Afrika*, kur. 1 & 3)

Dhana ya Mungu inajitokeza katika mashairi mengi ya Shaaban Robert ikitajwa kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja kuwaombea dua watu wengine, kujiombea dua yeye mwenyewe, ama kumsifu na kujaribu kumwelezea kwa watu wengine. Mathalani, baadhi ya mashairi ambayo ama humtaja Mungu, mbingu, au siku ya mwisho/siku ya hukumu, dhana ambazo zinahusishwa na Mungu moja kwa moja ni: *Tofauti* na *Tendo* katika *Mwafrika Aimba*; *Tegemeo, Sijafahamu* na *Matendo* na *Fidia* katika *Almasi za Afrika.*
Tumeona pia katika mifano kadha wa kadha hapo juu Shaaban Robert akimhusisha Mungu katika kila kitu. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Shaaban Robert, baada ya kufa binadamu huendelea kuishi katika roho mpaka siku atakaporudishiwa mwili ili kukabiliwa na adhabu au starehe ya peponi. Ikiwa

mtu alifanya makosa mbalimbali ataadhibiwa, na ikiwa alifanya matendo mazuri basi atatuzwa, ndio maana Shaaban Robert anasisitiza umuhimu wa kuishi vizuri ili mtu anayeishi vizuri akapate tuzo huko mbinguni badala ya kutupwa jehanamu ambako atateswa milele kama mashairi yake mengi yanavyosema. Mfano wa mashairi hayo ni: shairi la *Matendo na Fidia* na utenzi wa *Neema Nyingi Ajabu*. Kwa mfano, katika utenzi wake wa *Neema Nyingi Ajabu* anaeleza thawabu anayoipata mtu aliyefuata mafundisho ya dini baada ya kufa na adhabu inayotolewa kwa mtu ambaye hakuzingatia amri za Mungu na kutenda matendo mabaya alipokuwa akiishi hapa duniani:

*Adhabu iliyo kuu,*
*Ni moto chini na juu,*
*Haifai kusahau,*
*Kuwa hili litakuwa (Almasi za Afrika*, uk. 45*)*

*Dini anayefuata,*
*Njia njema atapita,*
*Na daraja ya sitara,*
*Kwake pana itakuwa (AF*, uk. 49*)*

Vilevile, katika utenzi huohuo anasisitiza kuwa macho na shetani kwa sababu shetani ana tabia ya kushawishi watu ili wafanye makosa yanayomchukiza Mungu. Mara baada ya kuanguka, yaani baada ya binadamu kufanya dhambi, shetani hukimbia na kumuacha binadamu katika dhambi kama utenzi unavyosema:

*Jihadhari na bilisi*
*Usimpe nafasi,*
*Ilinde yako nafsi,*
*Ama itaangamia,*

*Kuwa shetani huruka*
*Mtu [akishaanguka],*
*Ni neno lenye hakika,*
*Acha kumwandamia.* (*Alamsi za Afrika*, uk. 42)

Wakati Shaaban Robert anasema hivi, Mugyabuso Mulokozi katika shairi lake la *Kalale Mwenyewe* akiwa anazungumza na mtu aliyefariki dunia anasema:

*Bali ninajua uliko hakupo*
*Hakuna madai, hakuna malipo*
*Maisha ya mtu ni hapa alipo*
*Mengine hayapo, kiyama hakipo!* (*Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, uk. 68)

Mulokozi anaendelea kufafanua kuwa hizo dhana zinazotajwa zipo hapahapa duniani na anazifafanua kama ifuatavyo:

*Roho yako*
*Ndiyo Mungu wako*
*Mazingira yako*
*Ndiyo shetani wako*
*Kaburi lako*
*Ndiyo mbingu yako*
*Mateso yako duniani*

*Ndiyo jahanam yako.*
*Nimesema* (*Kunga ya Ushairi na Diwani Yetu* na *Mashairi ya Kisasa*, uk. 76 & 31)

Kwa hiyo, tofauti za kimtazamo zinaonekana bayana katika ushairi wao. Mugyabuso Mulokozi anaposisitiza matendo mema na kukemea mabaya hahusishi dhana ya maisha baada ya kifo ilhali Shaaban Robert anahusisha matendo mema na matendo mabaya na adhabu za hapahapa duniani na adhabu na thawabu za kiwango kikubwa zaidi, yaani adhabu ya moto ambayo haina mfano wake hapa duniani au kwenda peponi kwenye starehe kubwa kuliko zile zinazopatikana hapa duniani. Kwa mfano, katika mashairi yake kadhaa anadokeza wazo hilo, baadhi ya mashairi hayo *ni Matendo na Fidia* na *Neema nyingi Ajabu*. Kwa mfano, ubeti mmojawapo katika shairi la *Matendo na Fidia* msanii anasema:

*Mwenye matendo halali ana tuzo maridhawa,*
*Fidia aina mbili: moja katika dunia-*
*Na nyingine bilkuli peponi humngojea,*
*Maisha ni ya matendo na mauti ya fidia* (*Almasi za Afrika*, uk. 36)

Akihadharisha kwa wale wanaotenda maovu juu ya adhabu watakayoipata, Shaaban Robert katika utenzi wa *Neema nyingi Ajabu* anasema watu wanaofanya maovu watapata:

*Adhabu iliyo kuu,*
*Ni moto chini na juu,*
*Haifai kusahau,*
*Kuwa hili litakuwa* (*Almasi za Afrika*, uk. 45)

Katika utenzi huo anaendelea kusema kuwa ikiwa adhabu ndogondogo za hapa duniani kama vile kifungo na kuchapwa binadamu wanashindwa kuvumilia je, wataweza huo moto?

## 3.0 Mitazamo ya Washairi hawa Imeathiriwa na Falsafa Gani?

Kama tulivyodokeza hapo awali, Waafrika wameathiriwa na falsafa mbalimbali zikiwemo zile za Mashariki ya Mbali, Mashariki ya Kati, au falsafa za Kimagharibi, yaani zile za Ulaya na Marekani na falsafa za Kiafrika. Hata hivyo, hatuwezi kupinga ukweli kuwa Waafrika pia wameathiri mawazo ya wanafalsafa wa Kimagharibi[5]. Inawezekana pia mawazo ya malenga hawa

---

[5] Kwa mujibu wa George G. M. James, wanafalsafa wengi wanaopewa sifa kubwa duniani kama vile Thales, Anaximenes na Anaximander kama waanzilishi wa falsafa, na wengine wengi waliofuata baadaye, walipata elimu kutoka kwa viongozi wa dini wa enzi hizo huko Misri. Maandiko karibu yote yanayohusu

hayajaathiriwa na mitazamo mingine lakini kilichotokea ni kufanana kwa mawazo yao na mawazo yanayojitokeza katika jamii nyingine kwa wataalamu wengine au wameathiriwa na falsafa za nje. Katika makala haya tunaamini kuwa mawazo na mitazamo ya wataalamu hawa vimeathiriwa na falsafa kutoka nje ya Afrika. Kwa mfano, Mugyabuso Mulokozi kwa sifa za mashairi yake inaonesha kuwa ameathiriwa kwa kiasi kikubwa na falsafa za kijamaa na kisoshalisti, yaani falsafa za Karl Marx na Mao Tse Tung zinazopinga kwa dhati kabisa mifumo ya kinyonyaji kama ile ya kibepari na kikabaila. Ni falsafa hizihizi zinazopinga dini kwa sababu dini hupumbaza akili za watu na kudhoofisha harakati za kupigania haki wakiamini kuwa kuna nguvu zaidi ya binadamu inayoweza kuwasaidia, yaani Mungu.

Kwa mujibu wa Lobkowicz (1964) Karl Marx hakupinga dini kama zilivyopinga taasisi za kikomunisti au watu wengine kama Ludwig Feuerbach[6] na Bruno Bauer[7]. Ingawa Marx alikubaliana na Feuerbach kuwa Mungu ni dhana iliyoumbwa na binadamu, hakukubaliana na madai ya Ludwig Feuerbach wala ya Bruno Bauer kwa kutaka kuzuia kabisa uwepo wa dini. Karl Marx aliichukulia dini kuwa ni matokeo ya kitu kibaya zaidi ambacho ni ama kutokujitambua kwa binadamu au binadamu amejipoteza tena mwenyewe. Kwa hiyo, Marx alisisitiza kuondoa mfumo mbovu unaosababisha uwepo wa dini, baada ya kuuondoa huo mfumo, dini zitatoweka zenyewe (Wolff, 2001). Msigano huu baina ya dini na Umarx unatokana na harakati za Marx kutaka kuhamasisha mapambano dhidi ya unyonyaji wa kibepari ambapo anaona dini ni itikadi inayowalevya watu, badala ya kupambana na wanyonyaji, hufikiri kuhusu maisha ya peponi ambayo kwa madai yake ni mawazo tu ambayo binadamu alijiundia. Kutokana na maelezo hayo mafupi kuhusu Karl Marx na wenzake, tunaweza kusema kuwa mawazo yenye mwelekeo huu yamemwathiri Mugyabuso Mulokozi. Kwa hiyo, mawazo ya Mugyabuso Mulokozi yanayojitokeza katika mashairi yake ni mwendelezo wa falsafa ya Kimarx.

---

falsafa hayaelezi ukweli huu kuwa fikra zinazodaiwa kuzalishwa na Wayunani zilitokea Afrika. Ukimya huu ni mwendelezo wa fikra hasi dhidi ya Afrika zilizojengeka miaka mingi iliyopita kuwa Afrika ni bara la giza. Kwa maelezo zaidi juu ya madai haya soma James (1954).

6 Kwa mujibu wa Feuerbach, Mungu anayetajwa na Wayahudi na Wakristu ni mwendelezo wa ukamilifu wa binadamu mwenyewe. Sifa mbalimbali anazopewa Mungu kama vile upendo, wema, hekima, na uumbaji, ni dhana alizonazo binadamu. Kibaya zaidi katika Ukristu ni kupanuka kwa mawazo hayo na kuumba kitu kingine nje ya binadamu, yaani kuumba nafsi inayoitwa Mungu. Mungu huyo aliyeumbwa katika akili za binadamu anweza kuwaendesha binadamu kwa madai mbalimbali kama vile kukosa upendo, kutenda maovu, kufanya mambo ya kijinga ambavyo vinapingana kabisa na dhana chanya ambazo ni upendo, wema, hekima na uwezo anaopewa huyo mungu wa kubuni (Comstock, 1976).

7 Kwa upande wake, Bruno Bauer alipinga dini za Kiyahudi na Kikristu kuwa ni dini zinazopingana na ukombozi.

Kwa upande wa Shaaban Robert, kazi zake za ushairi zinaonekana kuwa amethiriwa na imani ya dini ya Kiislamu[8] kwa kiasi kikubwa. Kwa kuwa amekulia katika familia ya Kiislamu kwelikweli, kama wasemavyo Ulenge na Taib (2009). Msanii huyu anaiona dunia kwa kutumia macho ya dini ya Kiislamu. Mawazo mbalimbali ya Shaaban Robert yanapatikana katika falsafa ya dini ya Kiislamu. Shaaban Robert anaeleza sehemu za falsafa hii katika mashairi yake mengi. Kwa hiyo, tofauti kubwa baina ya Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert ni athari walizozipata kutoka katika makundi mawili yenye fikra tofauti. Kundi moja kutoka Mashariki ya Kati, lililoasisiwa na Mtume Muhamad ambao wanaamini kuwa binadamu ni tofauti na wanyama wengine hivyo akifariki dunia anaendelea kuishi, na kundi lingine kutoka nchi za Magharibi lililoasisiwa na Karl Marx na wenzake.

## 4.0 Hitimisho

Makala yetu imechunguza tofauti za mitazamo kuhusu falsafa ya maisha kama ilivyoelezwa na malenga wawili, wa Kiswahili kutoka Tanzania, yaani Mugyabuso Mulokozi na Shaaban Robert. Tumeona kuwa malenga hawa wanatofautiana kwa kiasi kikubwa huku wakikubalina katika masuala machache sana katika maeneo yaliyochunguzwa. Halikadhalika, tumebaini kuwa mitazamo yao kuhusu maisha na mustakabali wake imeathiriwa sana na falsafa kutoka nchi za Kimagharibi na Mashariki ya Kati. Bado kuna tofauti zaidi za kimaudhui na kifani zinazoweza kuchunguzwa baina ya malenga hawa wawili au kwa kuwalinganisha na waandishi au watambaji wa sanaa ya ushairi.

---

[8] Ni miongoni mwa imani za kidini zinazoamini kuwepo kwa maisha baada ya kifo. Mtu anayeishi baada ya kifo anaweza ama kuishi peponi au jehannam. Kuishi peponi ama jehannam kutokana na maisha ya binadamu hapa duniani, kama mtu aliishi vizuri kulingana na mafundisho ya dini ya Kiislamu basi ataenda mbinguni, na kinyume chake ataenda jehanamu. Dhana hizi za peponi na jehanamu zimetumiwa na Shaaban Robert zikiendana kabisa na mafundisho ya dini ya Kiislamu (Kvanvig, 2009). Kutokana na mafundisho ya Kiislamu kujitokeza kwa wingi katika kazi za Shaaban Robert, baadhi ya wahakiki wanapendekeza kazi za Shaaban Robert zihakikiwe kwa kutumia Mkabala wa Kiislamu (Taib (2008) katika Chuachua (2011)). Aidha, Taibu (2009) anasisitiza kuwa Shaaban Robert aliathiriwa na Uislamu kama anavyosema, "Kwa kweli dini ilikuwa msingi mkubwa uliomuongoza Sheikh Shaaban katika utunzi wake. Hata J. Mungai (1996) alimfahamu vyema Sheikh Shaaban katika maoni yake aliposema, 'Shaaban alikuwa si mwandishi aliyejiweza tu, bali mwandishi aliyeingiliwa sana na mila, dini na utamaduni wa Kiislamu.'" (Taib, 2009:143). Vilevile, Taib (2008) katika Chuachua (2011) anapendekeza kutumia mkabala wa Kiislamu katika uchanganuzi na uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili.

## Marejeo


Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory. Second Edition.* Manchester: Manchester University Press. Toleo la kwanza lilichapishwa mwaka 1995.

Beaty, J. A., Booth, J.P Hunter. K.J. Mays. (wah.) (2002). *The Norton Introduction to Literature Eighth Edition*. New York: W.W. Norton & Company.

Berryman Jr., S. (2010). "Democritus." *The Stanford Encyclopedia of Philosophy (Fall Edition)*, Edward N. Zalta (ed.), URL =<http://plato.stanford.edu/archives/fall2010/ entries/democritus/>.

Calder, T.C. (2007). "Is the Privation Theory of Evil Dead?" *American Philosophical Quarterly 44* (4): 371 – 381.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert.* Dar es Salaam: TUKI.

Comstock, R. (1976). "The Marxist Critique of Religion: A Persisting Ambiguity." *Journal of the American Academy of Religion, Juz. 44,* Na. 2: 327-342.

Courlander, H. (1996). *A Treasury of African Folklore*. New York: Marlowe & Company.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

_________(1977). Oral *Poetry: Its Nature, Significance and Social Context.* Cambridge: Cambridge University Press.

James, G. M. (1954). *Stolen Legacy.* New York: Philosophical Library.

Kvanvig, J. (2009). "Heaven and Hell." *The Stanford Encyclopedia of Philosophy (Fall Edition)*, Edward N. Zalta (ed.), URL = <http://plato.stanford.edu/archives/fall2009/ entries/heaven-hell/>

Lobkowicz, N. (1964). "Karl Marx's Attitude toward Religion." *The Review of Politics, Juz. 26,* Na. 3: 319-352.

Mbiti, J.S. (1990). *African Religions and Philosophy*. Oxford: Heinemann. Toleo la kwanza lilichapishwa mwaka 1990.

Mbiti, J.S. (1991). *Introduction to African Religion*. Oxford: Heinemann. Toleo la kwanza lilichapishwa mwaka 1975.

Milner, M. (1993). "Hindu Eschatology and the Indian Caste System: An Example of Structural." *The Journal of Asian Studies, Vol. 52,* Na. 2: 298-319. Ilisomwa 06/11/2012 < http://www.jstor.org/stable/2059649>.

Mulokozi, M. na K.K. Kahigi. (1973). *Mashairi ya Kisasa.* Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M. M. na K.K. Kahigi. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salaam: TPH.

______ (1995). *Malenga wa Bara*. Dar es Salaam: DUP. (Toleo la kwanza lilichapishwa na East African Literature Bureau, 1976).

Mulokozi, M.M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character, and Continuity*. Bloomington & Indianapolis: Indiana University Press.

Patton, W.M. (1900). "The Doctrine of Freedom in the Koran." *The American Journal of Semitic Languages and Literatures, Juz. 16*, Na. 3: 129-144.

Robert, S. (1959). *Insha na Mashairi*. Tanga: Art and Literature.

______ (1968). *Mashairi ya Shaaban Robert*. London: Nelson.

______ (1969). *Mwafrika Aimba*. London: Nelson.

______ (1972). *Almasi za Afrika*. London: Nelson.

Rosenberg, A.L. (2008). "Making the Case for Popular Songs in East Africa: Samba Mapangala and Shaaban Robert." *Research in African Literatures, Juz. 39 (3)*: 99-120.

Taib, A.H. (2009). "Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi." *Mulika Na. 28*: 131-147.

Wainwright, W. (2010). "Concepts of God", *The Stanford Encyclopedia of Philosophy (Winter Edition)*, Edward N. Zalta (ed.), URL = <http://plato.stanford.edu/archives/win2010/ entries/concepts-god/>.

Wolff, J. (2011) "Karl Marx", *The Stanford Encyclopedia of Philosophy (Summer Edition)*, Edward N. Zalta (ed.), URL = <http://plato.stanford.edu/archives/sum2011/entries/ marx/>.

Vázquez, A.S. (1973) *Art and Society: Essays in Marxist Aesthetics*. London: Merlin Press.